

# TANGAZO

## NAFASI ZA AJIRA KWA KADA ZA AFYA KWA MWAKA 2014/2015

Katibu Mkuu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii anapenda kuwaarifu Wizara imeanza zoezi la kuwapangiwa vituo vya vya kazi Wataalam wa Kada za Afya kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Wataalam wote waliopangiwa vituo vya kazi wanatakiwa kuripoti kwa waajiri wao ndani ya siku 14 tangu tarehe ya tangazo. Ifahamike kwamba hakutakuwa na utaratibu wa kubadilisha kituo cha kazi.

Waajiri wanakumbushwa kuwasilisha taarifa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu wataalam ambao hawajaripoti ili kuona uwezekano wa kujaza nafasi zao.

Vilevile, waajiri wanakumbushwa kukagua vyeti halisi vya kidato cha IV na VI, Vyeti vya taaluma na vyeti vya usajili (kwa wataalam wenye masharti ya usajili kwa mujibu wa miundo yao ya utumishi).

Orodha ya majina ya wataalam waliopangiwa kazi pamoja vituo walivyopangiwa inapatikana kwenye tovuti ya wizara [www.ehealth.go.tz](http://www.ehealth.go.tz). Wizara haitatoa barua za kupangiwa vituo vya kazi kama ilivyokuwa awali.

Wataalam ambao ni waajiriwa wa Serikali na kwa bahati mbaya wamepangiwa vituo vya kazi, wanatakiwa kubaki kwenye vituo vya awali. Pia, watumishi wanaofanya kazi kwenye mashirika ya dini na mashirika ya kujitolea ambao wanalipwa na mishahara na Serikali wanatakiwa kubaki kwenye vituo vyao.

Nawapongeza wataalam wote kwa kupata nafasi ya kutumia utaalam wenu katika kuwahudumiwa wananchi, na ninawatakia kazi njema na utumishi uliotukuka.

Imetolewa na:-

**Katibu Mkuu**

**Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii**

**06 Januari, 2015**